**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**HALMASHAURI YA MJI WA TARIME.**

SHULE YA SEKONDARI NKONGORE
S.L.P 466,
**TARIME.**
MOB: +255
10/12/2020.

**Kumb. Na NKSS/TTC/REG/ 5237**
**JINA A MWANAFUNZI**

**...........................................................**
**...........................................................**
**S.L.P....................................................**
**...........................................................**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

**UTANGULIZI**

Ninafurahi kukutaarifu kwamba, umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza January 2021 katika shule ya Sekondari Nkongore. Shule ya Sekondari Nkongore ipo Mtaa wa Kwigoronto kata ya Ketare , Halmashauri ya Mji wa Tarime na pia shule ipo umbali wa kilometa kumi (10) toka Tarime Mjini mwelekeo wa mlima chambiri.

Ili ufike Nkongore Sekondari panda bodaboda ambazo zinapatikana karibu na uwanja wa mpira wa Serengeti.

Shule hii ni kutwa, mchanganyiko wa Wasichana kwa Wavulana.masomo yanayo fundishwa ni tisa ambayo ni Fizikia, Kemia, Biolojia, Hisabati, Uraia, Kiswahili, Kiingereza, Historia na Jiografia.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 saa moja asubuhi, na unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25 / 01 / 2021.

**MAHITAJI MUHIMU YA KUZINGATIA**

**A. SARE YA SHULE**

**i. Wavulana**

- Suruali kwa wavulana yenye mikunjo (**turn up**) ya rangi ya **dark green**, mbili zenye mifuko mitatu na marinda mbili zisizo na madoido yoyote. Ni za kitambaa kizito cha suti ( suruali za modo hazitakiwi).
- Mkanda mweusi kwa wavulana wenye chuma cha kawaida na siyo vinginevyo.
- Shati nyeupe mbili mikono mifupi (Tetroni).
- Sweta la **dark green** lenye alama ya “V” shingoni.
- Viatu vyeusi vya kamba visivyo na madoido yoyote.
- Soksi nyeupe jozi mbili ndefu .
- Sare za michezo (Track suit ya rangi nyeusi yenye michirizi mieupe pembeni. )
- Viatu vya michezo (Raba)
-

ii. **Wasichana**

- Sketi kwa wasichana rangi **dark green** marinda box sita (6), sketi ndefu kuvuka goti na pindo la tumbo lisizidi **sm 5**, sketi fupi hazitaruhusiwa kamwe.
  ( sketi zote ziwe za kitambaa kizito cha suti)
- Blauzi nyeupe mbili mikono mifupi ( Tetroni).
- Sare ya michezo (Track suit ya rangi nyeusi yenye michirizi mieupe pembenmi )
- Viatu vya michezo (Raba )
- Sweta ya **dark green** yenye alama ya "V" shingoni.
- Viatu vyeusi vya kamba visivyo na madoido yoyote.
- Soksi nyeupe jozi mbili ndefu zinazofika kwenye magoti .

**NB**: wanafunzi wasicha wa KIISLAMU watavaa Sketi ya rangi **dark green** marinda box sita (6), sketi ndefu kuvuka goti na pindo la tumbo lisizidi **sm 5**, sketi fupi hazitaruhusiwa kamwe. na blauzi nyeupe mikono mirefu na kitambaa cha kichwani (Hijabu rangi nyeupe).

**Nimarufuku kuja na vipodozi shuleni.**
Msichana haruhusiwi kusuka nywele na kufuga nywele ndefu.

**B. MAHITAJI BINAFSI YA DARASANI**

i. Mathematical set ( Mkebe wa hesabu)
ii. Madaftari makubwa, yawe tisa ( Counter book 2 Quire)
iii. Begi dogo la kubebea madaftari (Usinunue mifuko ya nailoni "Pepsi")
iv. Kalamu ya wino.
v. Penseli.
vi. Rula moja.
vii. File yenye spring tags kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi.
viii. Aje na cheti cha kuzaliwa (Halisi na kivuli)
ix. Kamusi ya kiingereza.
x. Aje na kitabu cha kadi ya maendeleo ya mwanafunzi.

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995

Aidha inazingatia miongozo yote inayotelewa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi , yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi katika fomu ya kiambatisho A.

Unatakiwa kusoma mambo haya ya msingi, kisha utaweka saini yako pamoja na mzazi wako kuonesha kuwa umeelewa na kukubaliana nayo. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni ikiwa imesainiwa na mwanfunzi pamoja na Mzazi / Mlezi wake.

**MEDICAL EXAMINATION FORM.**

hii ni fomu ya maelekezo ya uchunguzi wa Daktari kuhusu hali ya afya ya Mwanafunzi. Fomu hii ijazwe na Daktari / Mganga mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara

utakaporipoti shuleni.

**KIPENGELE HIKI KIJAZWE NA MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI**

1. Mimi .......................................................................................... Mzazi / Mlezi wa mwanafunzi ............................................................................................ wa kidato cha kwanza 2021 ninakiri kuwa nimezisoma na kuzielewa sheria na kanuni zilizo elekezwa na uongozi wa shule na ninaahidi kwamba mwanangu atazifata kikamilifu kwa kipindi chote cha masomo yake.

   Saini ya **Mzazi /Mlezi ........................................................... tarehe ..................................**

**KIAMBATA "A"**

**SHERIA NA KANUNI ZA KUZINGATIA**

a) Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu viongozi wa Kitaifa, Wazazi, walimu na wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi wenzake na jamii inayoizunguka shule kwa ujumla.
b) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo darasani na nje ya darasa kulingana na ratiba ya shule.
c) Mwanafunzi anatakiwa kuwahi shuleni na kufanya shughuli zote atakazopewa na walimu wake wa masomo, zamu na darasa bila kukosa.
d) Mwanafunzi anatakiwa kufanyakazi zote za darasani, kazi ya nyumbani ( home work) na kazi mradi.
e) Mwanafunzi anatakiwa kuwepo shuleni muda wote wa masomo na asivuke eneo la shule bila ruhusa ya mwalimu.
f) Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia usafi wake wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule muda wote akiwepo shuleni.

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA MASOMO.**

i. Wizi wa mali ya umma/ wanafunzi wenzake.
ii. Uasherati na ushoga.
iii. Ubakaji.
iv. Matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, mirungi, marujuani na ulevi wa pombe.
v. Kupiga au kupigana.
vi. Kupata au kusababisha mimba.
vii. Kudharau bendera ya Taifa.

**"KARIBUNI SANA NKONGORE SEKONDARI"**

**.................................................**

**(MKUU WA SHULE)**

**TARIME TOWN COUNCIL**
**NYANDOTO SECONDARY SCHOOL**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

Full name.............................................................................................................................................

Age......................................................... Height ( in Cms) .................................................................

Weight...........................................................................................

1. Blood count............................................................... (Red and White) .........................................
2. Stool examination.........................................................................................................................
3. Urinalysis......................................................................................................................................
4. Syphilis and other V.D..................................................................................................................
5. T.B and Leprosy test.....................................................................................................................
6. Eye test.........................................................................................................................................
7. Ear.................................................................................................................................................
8. Chest.............................................................................................................................................
9. Abdomen......................................................................................................................................
10. Plano – test (girls).........................................................................................................................
11. Spleen...........................................................................................................................................

Addition information: e.g. Physical or impairments, infections, chronic or family disease (e.g. sickle cell) inability to certain food etc.

..........................................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................................

...........................................................................................................................................

I certify that the above named student is fit / is not fit to pursue Secondary Education.

Signature..................................................................... Date....................................

Designation...................................................................

Station.........................................................................